# GEITA LEO

## Toleo la Na. 11



Upanuzi wa kituo cha Afya Nyankumbu ambao umejumuisha ujenzi wa majengo sita ya kutolea huduma za afya ambayo ni jengo la wodi ya wazazi, jengo la upasuaji, jengo la maabara, jengo la kuhifadhia maiti, jengo la kufulia na nyumba ya mtumishi. Mradi huu umetekelezwa kwa Tsh. Milioni 500 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri .



Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Fulano ukiendelea, Shule hii inajengwa kwa Tsh. 600,000,000 kutoka Serikali kuu kupitia mradi wa SEQUIP katika eneo lenye zaidi ya ekari 9 ambalo limetolewa bure na Mhe. Boniphace Fulano Diwani wa kata ya Shiloleli.



Mradi wa Josho la kuoshea mifugo katika kata ya Bung'wangoko ambalo limejengwa kwa Tsh. 35,000,000 kutoka chanzo cha mapato ya ndani ya Halmashauri ya mji wa Geita.




Ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika zahanati ya Bombambili ambao umetekelezwa kwa Tsh. 50,000,000 kutoka Serikali kuu



Ujenzi wa shule ya msingi Bungwe kata ya Bulela ukiwa kwenye hatua ya ukamilishwaji, Shule ya msingi Bungwe inajengwa kwa Tsh.160,000,000 kupitia mradi wa wajibu wa kampuni kwa jamii ( CSR ) kutoka mgodi wa Dhahabu Geita.





Maendeleo ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja wa kisasa wa Michezo Magogo kata ya Bombambili ambao unajengwa kwa Tsh. 2,407,569,050.81 kupitia fedha za wajibu wa kampuni kwa Jamii ( CSR ) kutoka Mgodi wa GGM



Choo bora na cha kisasa chenye matundu 10 kwa ajili ya wanafunzi katika Shule ya msingi Nyabubele kata ya Kasamwa ambacho kimejengwa kwa Tsh. 10,000,000 kupitia fedha za huduma za kampuni kwa jamii kutoka Mgodi wa GGM





Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya mji Geita wakiwa kwenye mkutano wa kujadili utekelezaji wa Miradi ya maendeleo.



Ujenzi wa zahanati ya Mwamitilwa kata ya Kanyala ambao umetekelezwa kwa Tsh.50,000,000 za mapato ya ndani ya Halmashauri ya mji.



Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Rosemary Senyamule akizindua kampeni ya chanjo ya polio kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano mwezi mei 2022 katika Halmashauri ya mji Geita .





Upanuzi wa kituo cha Afya Mgusu ambapo jengo la Maabara na Wodi ya wazazi imekamilika pia jengo la upasuaji na nyumba ya watumishi ( three in one ) yanaendelea kujengwa. Mradi huu unatekelezwa  kwa Tsh.500,000,000 kutoka Serikali kuu  kupitia tozo za miamala ya simu.




Mkuu wa Wilaya ya Geita Mhe. Wilson Shimo akizungumza na wafanyabiashara wa eneo la Stendi ya mabasi Geita mjini ( hawapo pichani) akiwahamasisha kujenga desturi ya kufanya usafi wa mazingira mara kwa mara



Ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi katika Shule ya Sekondari Geita ukiwa kwenye hatua za ukamilishwaji, Mradi huu unatekelezwa kwa Tsh.160,000,000 kupitia Programu ya lipa kulingana na matokeo ( EP4R )



Jengo la utawala katika shule ya sekondari Nyanguku ambalo limejengwa kwa Tsh.60,000,000 kupitia fedha za huduma za kampuni kwa jamii ( CSR ) kutoka mgodi wa dhahabu wa Geita ( GGM)





Mmoja wa wakazi wa mtaa wa Wigembya kata ya Ihanamilo akichota maji safi na salama katika kisima kinachotumia umeme wa nguvu ya jua, Shughuli ya kutandaza mabomba itakapokamilika mradi huu utawanufaisha wakazi zaidi ya 2000 wa mtaa huo na maeneo ya jirani.



Kikosi cha timu ya Geita Gold Fc kikiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita Ndg. Zahara Michuzi na Makamu wa Rais Mwandamizi AngloGold Ashanti Tanzania na Ghana Ndg. Richard Jordinson.



Muonekano wa kuvutia wa Shule mpya ya Msingi Samina kata ya Mtakuja ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi, mchango wa Mbunge wa Geita Mjini na Tsh. 100,000,000 kupitia fedha za huduma za kampuni kwa jamii kutoka Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM).



Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Rosemary Senyamule (wa pili kutoka kulia safu ya kwanza ) akishiriki mazoezi ya viungo na baadhi ya Watumishi wa Umma, Sekta binafsi, Wanafunzi na Wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Geita.



Barabara ya Polisi hadi Rugembe yenye urefu wa KM 1 ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami nyepesi na mkandarasi Evax Construction Limited wa Muleba chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania ( TARURA ) Wilaya ya Geita



Ujenzi wa ofisi ya Mtaa wa Nyanza kata ya Kalangalala ambayo inajengwa kwa nguvu za wananchi pamoja na mapato ya mtaa. mpaka ukamilishaji wake itagharimu kiasi cha Tsh 50,000,000 .



Wajumbe wa kamati ya Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Geita wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Geita Mhe. Barnabas Mapande (aliyevaa kofia ) Wakikagua maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa michezo Magogo Geita Mjini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za MIkoa na Serikali za Mitaa Mhe. Innocent Bashungwa (wa pili kutoka kushoto safu ya kwanza) akishiriki uzinduzi wa kampeni ya usafi wa mazingira Geita Mjini pamoja na baadhi ya wakazi wa Mji wa Geita.



Muonekano wa shule mpya ya msingi Zanzui kata ya Buhalahala ambayo imejengwa kwa Tsh.250,000,000 kupitia fedha za huduma za kampuni kwa jamii ( CSR ) kutoka mgodi wa Dhahabu wa Geita katika eneo la ekari nane lililotolewa bure na Diwani wa kata ya Buhalahala Mhe.Dotto Zanzui Ludeha.



Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Mtakuja ikiwa kwenye hatua ya ukamilishwaji. Shule hii mpaka kukamilika kwake itagharimu kiasi cha Tsh. 160,000,000 kupitia fedha za huduma za kampuni kwa jamii ( CSR ) Kutoka Mgodi wa Dhahabu wa Geita.





Muonekano wa nje na ndani waJengo la Maabara lenye vyumba viwili kwa ajili ya Masomo ya Sayansi kwa vitendo. ujenzi wa maabara hii unaendelea kutekelezwa kwa Tsh.120,000,000 kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TEA).



Shughuli za ujenzi wa jengo la Utawala katika shule ya Sekondari Nyanza kata ya Kalangalala ukiendelea. Mradi huu unatekelezwa kwa Tsh. 89,880,714.29 kutoka TASAF kupitia fedha za programu ya Kupunguza Umaskini - Ujenzi wa Miundombinu.




Muonekano wa Madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Nyanguku yaliyojengwa kwa Tsh. 40,000,000 za Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19.

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Halmashauri ya Mji Geita
GEITA
TOWN COUNCIL

# HALMASHAURI YA MJI GEITA

TANZANIA
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa

Ndugu Mwananchi kumbuka kushiriki vyema zoezi la Sensa ya **Watu** na **Makazi** ifikapo tarehe **23. Agosti 2022.**

“Sensa kwa **Maendeleo**, Jiandae **kuhesabiwa**”

**Geita tupo tayari kuhesabiwa.**

Halmashauri ya Mji Geita

GEITA

TOWN COUNCIL




Jarida hili hutolewa bure kila baada ya miezi sita na Kitengo cha TEHAMA. Halmashauri ya Mji Geita. S.L.P 384 Geita Simu Na. 0282520437. Nukushi Na. 0282520347. Barua pepe : td@geitatc.go.tz, Tovuti : www.geitatc.go.tz